TANGAZO LA SERIKALI NA. 633 la tarehe 1/9/2023

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 29(1)(d))*

AMRI YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJISAFI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BARIADI YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurekebisha Bei za Huduma za Majisafi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi ya Mwaka, 2023.

Marekebisho ya bei

2. Bei za majisafi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi zinarekebishwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Amri hili.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) kabla ya kutoa ankara kwa mara ya kwanza kwa ajili ya matumizi ya bei na ada zilizoainishwa kwenye Amri hii, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi itapaswa kuwasilisha uthibitisho kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwamba iliwataarifu wateja wake kuhusu Amri mpya ya bei na kwamba iliwafahamisha ipasavyo wadau wake ikiwa ni pamoja na viongozi wa serikali, viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini, na wateja wake, kuhusu mabadiliko ya bei;

(b) ifikapo tarehe 30 Septemba, 2023 au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi itawasilisha kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa

masharti ya Amri hii;

(c) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi , kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(d) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi itahakikisha kuwa inafikisha na kuziunganisha na huduma ya maji taasisi zote za umma ikiwemo zahanati za Sanungu na Nyangaka, shule za msingi za Yoma, Sanungu, Izunya, Ngashanda, Nyangaka na Sima A na shule ya sekondari ya Chenge ifikapo tarehe 30 Juni, 2024;

(e) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi itatoa huduma ya maji kwa wakazi wote waishio kandokando ya vyanzo vya maji vya visima vya Isanzu, Izunya, Mahaha Na.1, Mahaha Na.2, Mahaha Na.3, Mahaha Na.4, , Mahina, Malinoni Na.2 na Malinoni Na.3 ifikapo tarehe 30 Juni, 2025;

(f) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi itaandaa na kutekeleza mpango wa kuwafikia wateja wote na kuwasilisha kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji taarifa ya utekelezaji wa mpango huo kila mwaka;

(g) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(h) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri hii ya Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Amri hii;

(i) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi itaendelea kuwasilisha kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji taarifa zake za fedha kama ilivyoidhinishwa katika Jedwali la Nne la Amri hii, na utendaji kwa mujibu

wa matakwa ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Taarifa hizi zitatumiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi ikilinganishwa na mamlaka nyingine za majisafi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake; na

(j) katika kuhakikisha kunakuwepo na huduma endelevu ya maji hususan kipindi cha kiangazi, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi inaelekezwa kuandaa na kutekeleza mpango wa kuvuna maji ya mvua.

Kufuta Amri Na. 11 – 014 ya 2011

4. [Amri hii inafuta Amri Na. 11-014 ya mwaka 2011].

---

MAJEDWALI

---

JEDWALI LA KWANZA.

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 660 | 1,118 | 1,206 | 1,229 |
| Taasisi | 780 | 1,322 | 1,426 | 1,452 |
| Biashara | 900 | 1,525 | 1,645 | 1,676 |
| Viwanda | 1,100 | 1,864 | 2,011 | 2,048 |
| Magati | 1,000 | 1,500 | 1,500 | 1,500 |
| WASTANI | 756.05 | 1,281 | 1,392 | 1,417 |

Jedwali Namba 1(b): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi kwa Unganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 33,000 | 26,000 | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji (Shilingi kwa Rejesho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 16,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 21,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | - | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

______

JEDWALI LA PILI

______

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(c))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| Miradi Itakayotekelezwa | Gharama (TZS) | | |
|---|---|---|---|
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Uwekezaji Mpya | | | |
| Kuongeza urefu wa mtandao wa mabomba kwa kilomita 10 yenye kipenyo cha milimita 32 mpaka 75 kwenye maeneo ambayo hayafikiwa na huduma (Sesele, Nyaumata, Nyangaka, Isanzu, and Majahida). Kilomita 2 mwaka 2023/24, kilomita 3.2 mwaka 2024/25 na mwaka 2025/26 kilomita 4.8 | 12,000,000 | 20,000,000 | 30,000,000 |
| Kufunga viungio mbalimbali na vifaa vya kurekebisha/kusaidia mzunguko na mgandamizo wa maji ifikapo Juni, 2025. Valvu 10 mwaka 2023/24, 50 mwaka 2024/25 na 50 kwa mwaka 2025/26 | 3,000,000 | 18,000,000 | 20,000,000 |
| Kununua dira za maji kwa ajili ya wateja wapya 1,200 kwa mwaka 2023/24, 1600 kwa mwaka 2024/25 na 2000 kwa mwaka 2025/26 | 149,760,000 | 207,667,200 | 269,967,360 |
| Kupanua mtandao wa maji kwa kulaza kilomita 40 za mabomba yenye kipenyo cha kati ya milimita 32 na 100 kwenda kwenye maeneo yasiyokuwa na huduma (Nyangaka, Nyakabindi, Bunamhala, Kisiwani, Isanga, Nyangokorwa, Mhango and Guduwi) na kwenye taasisi muhimu. Kilomita 6 kwa 2023/24; kilomita 12 kwa mwaka (2024/25) na kilomita 16 kwa 2025/26. | 35,680,726 | 215,725,379 | 337,090,886 |
| Kununua dira kubwa za maji 10 na kuzifunga kwenye mabomba ya kuchukua maji kutoka kwenye vyanzo vya maji, matanki ya maji na kanda za mtandao wa maji | - | 5,000,000 | 5,000,000 |
| Kujenga vituo 16 vya kutibu maji kwa kutumia chlorini kwenye matanki. Vituo vitatu(3) mwaka 2023/24, vitano (5) mwaka 2024/25 na nane (8) mwaka 2025/26 | 1,000,000 | 5,000,000 | 8,000,000 |
| Kutunza vyanzo vya maji kwa kuotesha miti | 1,800,000 | 6,500,000 | 5,000,000 |
| Kununua vitendea kazi vya ofisini ikiwemo kompyuta ya mezani (8) na mpakato (7). Kompyuta nne (4) mwaka 2024/25 na nne (4) mwaka 2025/26 | - | 16,000,000 | 18,000,000 |
| Kununua vifaa vya thamani vya ofisini ikiwemo viti, meza na makabati | - | 5,000,000 | 7,000,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 633 (Linaendelea.)*

| Miradi Itakayotekelezwa | Gharama (TZS) | | |
|---|---|---|---|
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Kununua pikipiki 6 kwa ajili ya wasoma mita. Moja mwaka 2023/24, mbili mwaka 2024/25 na tatu mwaka 2025/26 | 3,000,000 | 6,000,000 | 9,000,000 |
| Jumla Uwekezaji Mpya | 206,240,726 | 504,892,579 | 709,058,246 |
| Miradi ya Ukarabati | | | |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Majahida 1 | 2,869,760 | 2,984,550 | 3,103,932 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Majahida 2 | 2,869,760 | 2,984,550 | 3,103,932 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Majahida 3 | 3,864,684 | 4,019,271 | 4,180,042 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Ndoba | 2,869,760 | 2,869,760 | 2,869,760 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Kidinda 1 | 2,869,760 | 2,869,760 | 2,869,760 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Kidinda 2 | 2,869,760 | 2,984,550 | 3,103,932 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Isanzu 1 | 7,000,000 | 7,280,000 | 7,571,200 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Isanzu 2 | 8,500,000 | 8,840,000 | 9,193,600 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Isanzu 3 | 3,386,317 | 3,521,769 | 3,662,640 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Sanungu 1 | 2,869,760 | 2,984,550 | 3,103,932 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Sanungu 2 | 3,386,317 | 3,521,769 | 3,662,640 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Somanda 1 | 3,386,317 | 3,521,769 | 3,662,640 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Somanda 2 | 2,869,760 | 2,984,550 | 3,103,932 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Nyamhimbi | 3,386,317 | 3,521,769 | 3,662,640 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Izunya | 3,386,317 | 3,521,769 | 3,662,640 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Nyaumata | 3,386,317 | 3,521,769 | 3,662,640 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Mahina | 3,864,684 | 4,019,271 | 4,180,042 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Gitoya | 3,864,684 | 4,019,271 | 4,180,042 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Kigangoni | 2,869,760 | 2,984,550 | 3,103,932 |

*Tangazo la Serikali Na. 633 (Linaendelea.)*

| Miradi Itakayotekelezwa | Gharama (TZS) | | |
|---|---|---|---|
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Nyangaka | 2,869,760 | 2,984,550 | 3,103,932 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Malinoni 1 | 3,864,684 | 4,019,271 | 4,180,042 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Malinoni 2 | 3,864,684 | 4,019,271 | 4,180,042 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Malinoni 3 | 3,864,684 | 4,019,271 | 4,180,042 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Nanenane | 2,869,760 | 2,984,550 | 3,103,932 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Nanenane Gagabali | 2,869,760 | 2,984,550 | 3,103,932 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Nanenane JKT | 3,386,317 | 3,521,769 | 3,662,640 |
| Kubadilisha mota moja ya pampu kila mwaka kwenye kisima cha Nanenane Mwembeni | 3,601,662 | 3,745,729 | 3,895,558 |
| Kubadilisha mabomba machakavu yenye urefu wa kilomita 6 na kipenyo cha milimita kati 50 na 63 | 12,050,000 | 12,532,000 | 13,033,280 |
| Kubadilisha mabomba machakavu yenye urefu wa kilomita 6 na kipenyo kati ya milimita 32 na 50 | 9,232,000 | 9,601,280 | 9,985,331 |
| Kubadilisha mabomba ya zamani yenye urefu wa kilomita 8 na kipenyo cha milimita 32. | 9,702,000 | 10,090,080 | 10,493,683 |
| Kubadilisha valvu 33 zenye kipenyo kati ya milimita 100 hadi 200. Tisa (9) mwaka 2023/24, 11 kwa mwaka na 13 kwa mwaka 2025/26 | 7,488,000 | 9,301,760 | 11,248,640 |
| Kubadilisha geti valvu 264 zenye kipenyo cha kati ya milimita 90 na 32. Sabini (70) kwa mwaka 2023/24, 88 kwa mwaka 2024/25 na 106 kwa mwaka 2025/26 | 5,896,800 | 8,068,736 | 10,404,992 |
| Kubadilisha valvu za upepo 3 kila mwaka | 600,000 | 624,000 | 648,960 |
| Kubadilisha dira za maji chakavu 600, 150 kwa mwaka 2023/24, 200 kwa mwaka 2024/25 na 250 kwa mwaka 2025/26 | 20,220,000 | 27,958,400 | 36,245,920 |
| Kubadilisha dira kubwa za maji 36 zenye kipenyo cha milimita kati ya 75 hadi 150 kwenye mabomba ya vyanzo vya maji, 10 kwa mwaka 2023/24, 12 kwa mwaka 2024/25 na 14 kwa mwaka wa fedha 2025/26 | 2,700,000 | 3,364,800 | 4,077,024 |
| Kubadilisha dira kubwa za maji 30 zenye kipenyo kati ya milimita 100 hadi 160 kwenye mabomba ya vyanzo vya maji. Nane (8) kwa mwaka 2024/25, 10 kwa mwaka 2024/25 na 12 kwa mwaka 2025/26 | 4,656,000 | 6,048,800 | 7,544,102 |
| Jumla Miradi ya Ukarabati | 170,106,14 | 188,824,064 | 208,735,930 |

*Tangazo la Serikali Na. 633 (Linaendelea.)*

| Miradi Itakayotekelezwa | Gharama (TZS) | | |
|---|---|---|---|
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| | 5 | | |
| Jumla ya Uwekezaji Wote | 376,346,87 1 | 693,716,643 | 917,794,176 |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(g))*

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2023/24-2025/26)

| Maelezo | Kizio | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Idadi ya watu inayofikiwa na huduma ya maji | % | 75 | 80 | 95 |
| Maunganisho mapya ya majisafi | No | 1,200 | 1,600 | 2,000 |
| Upotevu wa Maji | % | 24 | 23 | 20 |
| Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja | % | 100 | 100 | 100 |
| Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato | % | 92 | 95 | 97 |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(h)*

MAPATO YANAYOHITAJIKA

| Marekebisho ya Mahitaji ya Mapato (TZS) | | | |
|---|---|---|---|
| Maelezo | Makisio | | |
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Gharama za Uzalishaji | 251,846,341 | 329,183,718 | 380,103,838 |
| Ukarabati na Matengenezo | 104,097,570 | 117,375,607 | 127,217,170 |
| Gharama za Kiiutumishi | 230,652,420 | 267,801,210 | 287,541,390 |
| Gharama za Kiutawala | 116,573,742 | 133,022,476 | 139,734,345 |
| Gharama za Matangazo | 11,100,000 | 16,200,000 | 19,200,000 |
| Gharama za Matukio na Ufadhili | 3,400,000 | 3,400,000 | 3,400,000 |
| Gharama za Bodi | 63,362,300 | 65,143,700 | 66,925,100 |
| Gharama za Utunzaji wa Fedha | 1,200,000 | 1,200,000 | 1,200,000 |
| Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo | 782,232,370 | 933,326,710 | 1,025,321,840 |
| Uwekezaji wa Miundombinu Mipya | 206,240,730 | 504,892,580 | 709,058,250 |

*Tangazo la Serikali Na. 633 (Linaendelea.)*

| Marekebisho ya Mahitaji ya Mapato (TZS) | | | |
|---|---|---|---|
| Maelezo | Makisio | | |
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Ukarabati na Kubadili Miundombinu | 170,106,150 | 188,824,060 | 208,735,930 |
| Mapato Yote Yanayohitajika | 1,158,579,240 | 1,627,043,350 | 1,943,116,020 |
| Ondoa: | | | |
| Ada ya Maunganisho Mapya | 31,200,000 | 41,600,000 | 52,000,000 |
| Ada ya Kurejesha Huduma | 2,311,138 | 3,039,198 | 3,949,274 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Maji | 1,125,068,100 | 1,582,404,150 | 1,887,166,750 |

Dodoma,
................., 2023

JAMES A. MWAINYEKULE,
*Mkurugenzi Mkuu*